

KWA WARUMI. XV.

- 17 Nina kujisifu katika Masiya Isa kwa Mu-  
18 ungu, kwani sitathubutu kutoa neno asiloli-  
tenda Masiya kwa mimi, mataifa watii kati-  
19 ka na neno na tendo, kwa nguvu ya ishara  
na ajabu, kwa nguvu yake Roho Mtakatifu,  
hatta mimi, kutoka Yerusalemi na kuzu-  
nguka katta katika Illuriko, nimetimiliza  
20 anjili yake Masiya, nikiona kazi ya heshima  
ndiyo, kuhubiri pasiponenwa jina lake Ma-  
siya, nisijenge juu ya msinji wa mwenyewe,  
21 lakini kama ilivyoandikwa, Wasiohubiriwa  
mambo yake wataona, na wasiosikia, wata-  
22 fahamu. Kwa hiyo nikazuiwa sana katika  
kuja kwenu.
- 23 Sasa nisipokuwa tena na nafasi katika  
inchi hizi, nikiwa tangu miaka mingi na  
24 shauko kuja kwenu, nikisafiri kwenda Spa-  
nia, nataraja katika kupita kuwaona ninyi,  
na kupelekwa mbele nanyi, nikishibishwa  
kadiri kwanza nanyi.
- 25 Illa sasa nakwenda Yerusalemi nikiwa-  
26 ngojea watakatifu. Kwani Umakedoni na  
Akaya wamependezwa kufanya usharika nao  
walio maskini wa watakatifu walioko Ye-

KWA WARUMI. XVI.

- 27 rusalemi. Wamependezwa, nao imewapasa, kwani mataifa wakishariki nao mambo ya roho, imewapasa kuwachukulia mizigo katika mambo ya mwili.
- 28 Nikitimiza haya, nikiwawekea kwa muhuri tunda hili, nitasafiri kwa ninyi kwenda
- 29 Spania. Najua nikija kwenu, nitakuja katika kujaa mbaraka wake Masiya.
- 30 Nawasihi ninyi, ndugu, kwa Bwana wetu Isa Masiya, na kwa mapenzi yake Roho, mjitahidi pamoja nami, katika kumwomba
- 31 Muungu kwa ajili yangu, niokoke katika wale wasioamini wa Uyahudi, na ungoje wangu ulio katika Yerusalemi ukubalike nao
- 32 watakatifu, nipate kuja kwenu furahani, kwa kupenda Muungu, nipumzike pamoja nanyi.
- 33 Muungu wa amani pamoja nanyi nyote, amin.
- XVI. Nawaletea ninyi Foibe ndugu yetu, akiwa mngoje wa kanisa lilioko Kenkree, 2 mmkubali katika Bwana, kama ilivyowapasa watakatifu, mkamsayidie katika neno lo lote atakalowahitajia, kwani na yeye ame-

## KWA WARUMI, XVI.

Cambridge University Library  
www.lib.cam.ac.uk/is

kuwa msayidia wengi hatta na mimi.

- 3 Salimieni Priska na Akula watendao kazi  
4 nami katika Masiya Isa, waliolaza mashi-  
ngo yao kwa ajili ya maisha yangu, nisio-  
washukuru mimi tu, illa makanisa yote ya  
mataifa, nalo kanisa katika nyumba yao.
- 5 Salimieni Epaineto nimpendaye, aliye wa  
6 kwanza wa Asia kwa Masiya. Salimieni  
7 Maryamu, aliyetutendea kazi nyingi. Sa-  
limieni Androniko na Yunia, jamaa zangu  
waliofungwa pamoja nami, walio wa heshi-  
ma nao mitume, walionitangulia mimi kuwa  
katika Masiya.
- 8 Salimieni Amplia nimpendaye katika  
9 Masiya. Salimieni Urbano atendaye kazi  
pamoja nami katika Masiya, na Stakus ni-  
10 mpendaye. Salimieni Apelle aliyekubalika  
katika Masiya. Salimieni wale kwa Ari-  
11 stobulo. Salimieni Herodioni jamaa yangu.  
Salimieni walio wa Narkisso walio katika  
12 Masiya. Salimieni Trufajna na Trufosa,  
watendao kazi katika Masiya. Salimieni  
Persi aliyependwa, aliyetenda kazi nyingi  
13 katika Masiya. Salimieni Rufo mteule ka-

Cambridge University Library  
43  
www.lib.cam.ac.uk/is

KWA WARUMI. XVI.

Cambridge University Library

- 14 tika Masiya, na mama yake na yangu. Salimieni Asunkrito, Flegoni, Herme, Patroba, Herma, nao ndugu walio pamoja nao.
- 15 Salimieni Filologo, na Yulia, na Nereu, na ndugu yao, na Olumpa, nao watakatifu wote walio pamoja nao.
- 16 Msalimiane kwa busu takatifu. Makanisa yote yake Masiya wawasalimia.
- 17 Nawasihi, ndugu, angalieni wale wafanyao fitina na machukizo juu ya mafundisho
- 18 mliyojifunza, ukawageukie, kwani ndio wasiomtumikia Bwana wetu Masiya, illa matumbo yao wenyewe, na kwa maneno mazuri na mazumgumzo mema wapoteza mioyo yao
- 19 wajinga. Kwani mutia wenu umewafikia wote, juu yenu nafurahi, nataka'mwe werevu katika mema, na wajinga katika mabaya.
- 20 Muungu wa amani atamvunja Shetani chini ya miguu yenu upesi. Neema ya Bwana wetu Isa Masiya kwenu.
- 21 Timoteo atendaye kazi pamoja nami awasalimia, na Lukio, na Yaso, na Sosipatro,
- 22 jamaa zangu. Nawasalimia mimi Tertio
- 23 niandikaye waraka huu katika Bwana, awa-

44  
Cambridge University Library

www.lib.cam.ac.uk/is

## KWA WARUMI. XVI.

- salimia Gayo mwenyeji wangu na wa kanisa  
lote. Awasalimia Erasto wakili wa mji, na  
24 Kwarto ndugu. Neema ya Bwana wetu Isa  
Masiya nanyi nyote. Amin.
- 25 Awezaye kutufanya imara kwa anjili ya-  
ngu na kumhubiri Isa Masiya, kwa ufunuo  
wa siri isiyonenwa tangu zamani za milele,  
26 imethihirishwa kwa maandiko ya nabii, kwa  
amri yake Muungu wa milele, ikajulikani-  
27 shwa kwa mataifa yote, imani itiiwe, Muu-  
ngu mwenyi peke yake hekima, kwa Isa  
Masiya awe na utukufu hatta milele.  
Amin.

MWISHO.

